Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mwanafunzi _____

Tarehe _____

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA: 1 ¾

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1
MUDA : 1 ¾

MAAGIZO
Andika insha mbili . Insha ya kwanza ni ya lazima. Chagua Insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizosalia. Kila Insha isipungue maneno 400. Kila Insha ina alama 20.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

1. Insha ya lazima.
   Wewe umeteuliwa kama katibu wa jopo linalojadili matatizo yanayokumba kikosi cha polisi nchini Kenya, na kutoa suluhisho kwa matatizo hayo. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

2. Nchi nyingi za Afrika zimekabiliwa na mizozo inayoelekea kuzusha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Fafanua chanzo na matokeo ya mizozo hii.

3. Aumwaye na nyoka akiona ung'ong'o hushtuka.

4. Saa tatu asubuhi zilinipata ndani ya Afisi ya mwalimu mkuu. Ilikuwa ni siku moja tu baada ya matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne kutangazwa. Bwana Mengo alinitizama kwa macho ya huruma. Alichotamka kilitafuna maini yangu. Kijasho chembamba kikanipita. Wosia wa aliyekuwa mwalimu wetu wa darasa kuhusu udanganyifu katika mitihani ukarejea kwa akili yangu …… (Endeleza)

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Hii in Insha ya kumbukumbu.
   (i) Kichwa – Jina la mkutano, mahali, wakati, tarehe, saa n.k
   (ii) Orodha ya waliohudhuria.
   (iii) Orodha ya waliokosa kuhudhuria bila udhuru.
   (iv) Waliotuma udhuru.
   (v) Orodha ya waalikwa.

Ajenda
- Wasilisho / kufunguliwa kwa mkutano.
- Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za awali.
- Yaliyotokana na kumbukumbu za awali.
- Ajenda za siku.

Maudhui
(a) Matatizo
- Mazingira duni ya kikazi.
- Mkabala usiofaa miongoni mwa Askari.
- Mishahara duni.
- Ukosefu wa vipindi vya ushauri wa maelekezo kwa Askari.
- Miundo misingi mibaya k.m barabara mbovu.
- Vifaa vilivyopitwa na wakati

Mwalimu ahakiki hoja zingine mwafaka.

(b) Suluhisho
- Kuboresha mazingira ya kazi.
- Kuongezwa kwa mishahara.
- Kuteuliwa kwa maafisa wa uhusiano mwema miongoni mwa Askari.
- Kuboresha miundo misingi.
- Kununua vifaa vya kisasa.
- Kutenga wakati wa vipindi vya mashauri.

JINSI YA KUTUZA

Maudhui : Matatizo hoja 4 x 2 = 8
Suluhisho hoja 4 x 2 = 8
Sura = 4
20

Kijitabu hiki kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

Kuadhibu

- Akikosa kuzingatia sura – Ondoa alama 4.
- Asipozingatia urefu unaofaa – Ondoa alama 2.
- Makosa ya sarufi : Ondoa ½ alama kwa makosa 6.
- Makosa ya hijai: Ondoa ½ alama kwa makosa 6.

2. Hii ni Insha ya maelezo

Maudhui

Chanzo

- Tamaa ya uongozi.
- Ukabila.
- Tofauti za kiuchumi.
- Tofauti za mielekeo ya kisiasa.
- Wanasiasa kutovumiliana.
- Mifumo ya uchaguzi isiyofaa
- Hitilafu za katiba.

Matokeo

- Vifo.
- Uharibifu wa mali.
- Kudidimia kwa viwango vya uchumi.
- Kusababisha uyatima.
- Kuzorotesha misingi ya elimu.
- Ukimbizi wa ndani kwa ndani.
- Njaa na umaskini.

KUTUZA

Maudhui

Hoja 4 za chanzo
Hoja 4 za matokeo } x 2 = 16
Sura alama 4

Makosa ya sarufi ondoa ½ kwa makosa 6 = alama 3

Hijai ondoa ½ kwa makosa 6 = alama 3

Mwanafunzi asiyezingatia urefu – Ondoa alama 2

3. Hii ni insha ya methali

Maana ya methali (a) Nje
(b) Ndani
(c) Matumizi

- Mtahiniwa aandike kisa cha kudhihirisha ukweli wa methali hii.
- Aonyeshe ubaya uliotokea m.f ubakaji.
- Hatua alizochukua.
- Aseme pia jambo lililomshtuana
- Aonyeshe jinsi alivyojiandaa kukabiliana na shida hiyo.

Tazama

- Si lazima kuwa na kichwa.
- Maana ya nje na ndani zisizoafikiana katika utangulizi ni kosa ndogo la maudhui.
- Si lazima atangulize kwa maana ya nje na ndani.
- Tafsiri ikiwa sawa na kichwa kisithibitishe ukweli wa methali . Hii itakuwa kosa la kimaudhui.
- Anayenakili kichwa na kukosa kushughulikia mada itachukuliwa kuwa amejitungia swali na kulijibu.

4. Hii in Insha ya mdokezo.

- Mwanafunzi aanze kwa mdokezo alioupewa, akibadilisha atakuwa amejitungia swali, apoteze alama 4.
- Swali linakadiria uwezo wa mwanafunzi kubuni kisa kitakachoanzia kwa maneno aliyopewa.
- Mwanafunzi asianze kwa maneno tofauti bali hayo aliyopewa.
- Maudhui yaoane na maneno ya utangulizi.
- Masaibu ya kufutiliwa mbali kwa matokeo ya mtihani.
- Yaliyofanya mtihani kufutiliwa mbali.
- Msisimko kwa wanafunzi.
- Hatua zilizochukuliwa.

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mwanafunzi _____

Tarehe _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA: 2 ½

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2
MUDA : 2 ½

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SEHEMU	UPEO	ALAMA
UFAHAMU	15	
UFUPISHO	15	
MATUMIZI YA LUGHA	40	
ISIMU JAMII	10	
JUMLA	80	

Kijitabu hiki kina kurasa 9 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Wanafunzi wengi hutumia muda wao mwingi shuleni. Baadhi yao huwa katika shule za mabweni ambapo wanakaa muda wa miezi tisa au zaidi kwa mwaka. Wale ambao hawalali pia huwa shuleni kutoka asubuhi hadi jioni kwa muda usiopungua miezi tisa kwa mwaka.

Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kwamba wanafunzi wengi hawajali mazingira yao. Kuna baadhi ya shule ambazo huwa na majani makavu ambayo yametapakaa kila pahali. Wengine hutupa karatasi za kufunga vyakula ovyo ovyo na hali hii inaishia kwa kufungamana kwa mitaro ya maji taka.

Isitoshe, kuna baadhi ya wanafunzi ambao hawazingatii majukumu ambayo wamepewa ya kuweka mazingira ya shule katika hali ya usafi. Kwao, kufagia ama kuokota takataka shuleni ni kazi duni ambayo huichukulia ni ya vijakazi na wapagazi.

Wakati mwingine, juhudi za wanafunzi za kuweka mazingira ya shule katika hali ya usafi zinatungwa na hali duni ya majengo na vifaa vingine vinavyotumika katika mazingira ya shule.

Mazingira chafu husababisha kuzuka kwa magonjwa ya aina mbali mbali miongoni mwa mwanafunzi. Magonjwa yanayotokana na mazingira machafu ni kama vile kikohozi, kutapika, kuhara na magonjwa ya macho. Mazingira kama hayo pia hutatiza usomaji miongoni mwa wanafunzi. Zaidi ya hayo walimu nao hupoteza motisha ya kufundisha na jamii kwa jumla hufadhaishwa na mazingira ya aina hiyo.

Wanafunzi wanaokulia katika mazingira ya aina hiyo huinukia kuwa wananchi ambao hawajali mazingira na majukumu yao. Mazingira machafu pia huwa ni ishara ya kuporomoka kwa nidhamu shuleni. Mazingira kama haya huwa hatari kwa wanafunzi, walimu na jamii nzima. Si ajabu kwamba washikadau katika elimu hawana budi kupanga mikakati kabambe kuhakikisha kwamba mazingira safi shuleni yanadumishwa kwa manufaa ya wote wanaohusika.

Kuna njia nyingi za kudumisha mazingira safi. Baadhi yake ni kugawa majukumu ya kudumisha mazingira safi kati ya wanafunzi. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhakikisha kwamba anatekeleza wajibu wake wa kufagia na kuokota taka shuleni kama alivyopangiwa. Wale ambao wanakosa kufanya kazi yao, wanapaswa kuchukuliwa hatua kali ili wawe kielelezo kwa wengine wasiwaige. Kwa wembe huo huo, wale wanatekeleza wajibu wao ipasavyo wanapaswa kutuzwa ili nao wawe mfano mwema kwa wengine.

Halmashauri ya shule nayo ina jukumu la kukarabati majengo ya shule ili yatumike ipasavyo. Mapipa ya kutupa taka nayo yapaswa kuwekwa katika sehemu zilizotengwa ili wanafunzi waweze kuyatumia kutupa taka zao. Wanafunzi nao wanapaswa kuhimizwa kutumia mapipa hayo ifaavyo.

Mifereji ya maji taka nayo yapaswa kusafishwa ili isifungike. Mbinu hizi zote zikizingatiwa, mazingira safi yaweza kudumishwa katika shule kwa manufaa ya wote wanaoishi katika mazingira hayo.

UFAHAMU

Maswali

(a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka. (alama 1)

_____

_____

_____

(b) Thibitisha kauli kuwa wanafunzi wengi hawajali mazingira yao. (alama2)

_____

_____

_____

_____

(c) Uchafu wa mazingira shuleni hutokana na nini. (alama 2)

(d) Mazingira machafu huwa na madhara gani kwa maisha ya wanafunzi? (alama 3)

(e) Eleza namna usafi wa mazingira shuleni unavyoweza kudumishwa. (alama 3)

(f) Eleza istilahi zifuatazo kama zilivyotumiwa makalani. (alama 4)

(i) Washikadau

(ii) Mpagazi

(iii) Kukarabati

(iv) Mikakati

SWALI LA 2

MUHTASARI

Soma habari hii kisha ujibu maswali yanayofuata.

Maswala kadha yalijitokeza katika Kongamano la wanaume wanaopinga dhuluma ya kijinsia lililoandaliwa mjini Lilongwe, Malawi, mwezi wa Disemba.

Washiriki, wakiwemo wanaume na wanawake wachache wa umri tofauti na wanaofanya kazi mbalimbali walijadili hoja tofauti.

Hatimaye, ilidhihirika kuwa katika nchi zote nne; Kenya, Malawi, Ethiopia na Zambia, hakuna sheria maalumu za kuwashtaki na kuwahukumu wanyanyasaji wa kijinsia.

Kwa mfano, sharti la kupata ruhusa ya mkurugenzi wa mashtaka ya umma kuanzisha shtaka hilo linachukua muda mrefu na vikwazo vingi. Ingawa sheria ziko, watu wengi hawazifahamu wala kuweza kupata huduma za kisheria.

Ilijitokeza kuwa baadhi ya mila na tamaduni zinazoendelezwa katika eneo hili ni kinyume cha sheria na haki za binadamu. Mfano ni tohara ya wanawake na wasichana, ndoa za mapema, urithi wa wajane kwa lazima na unyakuzi wa mali waliyoachiwa. Kadhalika, ilidhihirika kuwa vyombo vya habari, wanasheria, wahudumu wa afya na viongozi wa kitamaduni hupuuza kesi za unyanyasaji wa kijinsia wakidai hayo ni matukio ya kawaida ya nyumbani.

Kongamano hilo pia lilieleza dhuluma ya jinsia inayoongeza umaskini na kueneza ukimwi. Suluhisho lililopendekezwa ni kumaliza ukatili huo na kuinua maendeleo na pato la jamii.

Pia washiriki walisema wanaume hawajihusishi kikamilifu katika jitihada za kumaliza dhuluma ya jinsia wala kusaidia kuwatunza wanaoambukizwa ukimwi.

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ya Kongamano hili. Serikali na Bunge katika eneo hili kubuni haraka na kutekeleza sheria za kusimamia na kudhibiti dhuluma ya jinsia ili kuangamiza kuenea kwa ukimwi.

Wananchi wachunguze kwa makini kutekelezwa kwa sheria hizo na kuhimiza serikali kutilia maanani haki za wanawake na binadamu kwa jumla. Katika kuendeleza sera za kitaifa za kijinsia, wizara ya jinsia ishirikiane na wizara zingine kuwasaidia waathiriwa kama kuwatibu na kuwashauri na kuwapa makao ya muda kesi hiyo ikiendelea. Kila mwananchi aelezwe kuwa dhuluma ya kijinsia inayotendwa na wanaume au wanawake ni ukiukaji wa sheria.

2. Muhtasari

Maswali

(a) Eleza kwa maneno 75 sababu zinazochangia dhuluma ya kijinsia kwa mintaarafu ya taarifa uliyosoma. (alama 6)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Nakala safi

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(b) Fafanua suluhisho zilizopendekezwa katika Kongamano lililotajwa katika taarifa.
(Maneno 65-70) (alama 6)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Nakala safi

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

3. MATUMIZI YA LUGHA.

(a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya koloni. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(b) Tunga sentensi ukitumia kitenzi <u>hubiri</u> katika kauli ya kutendesha. (alama 2)

_____

_____

_____

(c) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali.

Opembe alisoma kwa bidii ilhali hakupita mtihani. (alama 5)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(d) (i) Kishazi ni nini? (alama 2)

_____

_____

_____

(ii) Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuatayo .

Alipofika nyumbani alipumzika. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(e) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Karatasi

_____

_____

_____

(ii) Mama

_____

_____

_____

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinifu. (alama 2)
Usipolipa usiingie ndani.

_____

_____

_____

(g) Andika udogo na ukubwa wa sentensi hii. (alama 4)
Mbuzi aliuawa na mwizi huyo.
(i) Udogo

_____

_____

_____

(ii) Ukubwa

_____

_____

_____

(h) Taja sauti mbili za kaakaa ngumu. (alama 2)

_____

_____

_____

(i) Ziweke nomino zifuatazo kwa ngeli zake. (alama 2)
(a) Nge

_____

_____

_____

(b) Gofu

_____

_____

_____

(j) Ondoa ‘amba’ bila kubadilisha maana . (alama 2)
Mwanafunzi ambaye huchelewa huadhibiwa.

_____

_____

_____

(k) Andika katika usemi halisi. (alama 3)
Juma alimwomba Mutiso aende mahali alipokuwa ili amtume.

_____

_____

_____

(l) Tunga sentensi sahihi kubainisha maana ya vitate vifuatavyo. (alama 2)

(i) Hadaa

_____

_____

_____

(ii) Andaa

_____

_____

_____

(m) Tunga sentensi ukitumia neno “ila” kama: (alama 2)

(i) Nomino

_____

_____

_____

(ii) Kiunganishi

_____

_____

_____

(n) Andika visawe vya maneno haya. (alama 2)

(i) Mamba _____

(ii) Mviringo _____

(o) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo. (alama 3)

(i) Taarifa

_____

_____

_____

(ii) Msamaha

_____

_____

_____

(iii) Toba

_____

_____

_____

(p) Sahihisha sentensi hii.

Mahali huku pana wadudu wengi. (alama 1)

_____

_____

_____

4. ISIMU JAMII

Taja na kueleza sababu zozote tano zilizochangia maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru hadi sasa. (alama 10)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA: 2 ½

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. UFAHAMU

(a) Mazingira safi shuleni
Usafi wa mazingira shuleni (alama 1)

(b) - Baadhi ya shule huwa na majani makavu yaliyotapakaa kila mahali.
- Wengine hutupa karatasi za kufunga vyakula ovyo.
- Wanafunzi wengine hawazingatii majukumu yao.

Zozote 2 x 1 = alama2

(c) - Mapuuza kuwa kufagia ni kazi duni.
- Kutowajibika.
- Hali duni ya mijengo na vifaa vingine vinavyotumika katika mazingira ya shule.

Zozote 2 x 1 = alama 2

(d) - Husababisha kuzuka kwa magonjwa ya aina mbalimbali kama vile kikohozi,kutapika, kuhara na magonjwa ya macho
- Mazingira machafu hutatiza usomaji miongoni mwa wanafunzi.
- Walimu hupoteza motisha ya kufundisha.
- Jamii hufadhaishwa na mazingira machafu.

Zozote 3 x 1 = alama 3

(e) - Kugawa majukumu ya kudumisha usafi wa mazingira kati ya wanafunzi.
- Kuadhibu wanaokwepa majukumu yao.
- Kutuza wanaotekeleza wajibu wao.
- Halmashauri ya shule kukarabati majengo ya shule ili yatumike ipasavyo.
- Mifereji ya majitaka nayo kusafishwa ili isifunguke.

Zozote 3 x 1 = alama 3

(f) - Washikadau – wanaohusika
- Mpagazi – anayebeba mizigo
- Kukarabati – tengeneza upya kitu kilichoharibika .
- Mikakati – Mbinu / mipango inayotekelezwa kwa makini kabisa. (4 x 1 = 4)

Utuzaji
Hijai

Adhibu makosa ya hijai (h) yanapotokea mara ya kwanza hadi makosa sita (alama 3)

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

Sarufi

Adhibu makosa ya sarufi (s) yanapotokea kwa mara ya kwanza bora usiadhibu zaidi ya nusu ya alama zilizotuzwa.

2. **MUHTASARI**

(a) - Mashitaka dhidi ya dhuluma za Kijinsia yanachukua muda mrefu na vikwazo vingi.
- Watu wengi hawazifahamu sheria zinazohusiana na dhuluma za Kijinsia.
- Watu wengi hawapati huduma za kisheria zinazohusiana na dhuluma za Kijinsia.
- Hakuna sheria maalumu za kuwashtaki na kuwahukumu wanyanyasaji wa Kijinsia.
- Mila na tamaduni zinazoendelezwa ni kinyume cha sheria na haki za binadamu.
- Vyombo vya habari, wanasheria, wahudumu wa afya na viongozi wa kitamaduni hupuuza kesi za unyanyasaji wa Kijinsia wakidai hayo ni mambo ya kawaida ya kinyumbani.

Zozote 6 x 1 = 6

(b) - Serikali na bunge kubuni haraka na kutekeleza sheria za kusimamia na kudhibiti dhuluma ya kijinsia.
- Wananchi wachunguze kwa makini kutekelezwa kwa sheria hizo.
- Wananchi wahimize serikali kutilia maanani haki za wanawake na binadamu kwa jumla.
- Wizara ya jinisia ishirikiane na wizara zingine kuwasaidia waathiriwa kwa kuwatibu.
- Wizara ya jinsia iwape makao ya muda waathiriwa kesi zinapoendelea.
- Wizara ya jinsia iwashauri waathiriwa.
- Wananchi waelezwe kuwa dhuluma dhidi ya jinsia yoyote ni ukiukaji wa sheria.

Zozote 6 x 1 = 6
Utiririko alama 3

Utuzaji

Hijai (h)

Adhibu makosa ya hijai yanapotokea mara ya kwanza hadi makosa sita. (alama 3)

Sarufi (s)

Adhibu makosa ya sarufi yanapotokea kwa mara ya kwanza bora usiadhibu zaidi ya nusu ya alama zilizotuzwa.

Ziada

Adhibu maneno 10 ya kwanza ya ziada (Z) kisha baadaye uadhibu ½ alama kwa kila maneno matano ya ziada.

Tuza alama 3 za utiririko kulingana na unadhifu wa kazi ya mwanafunzi, mtiririko wa hoja, hati nzuri n.k

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) - Kuorodhesha
- Kusisitiza jina / jambo la pekee
- Dayalojia
- Kuonyesha saa / dakika
- Kunukuu vifungu vya maandishi ya kidini

Zozote 2 x 1 = alama 2

(b) Mf. Askofu aliwahubirisha makasisi hao siku ya Jumapili. (alama 2)

(c)

S					
S_1			U	S_2	
KN	KT		KT		
N	T	E		T	N
Opembe	alisoma	kwa bidii	ilhali	hakupita	mtihani

(alama 5)

(d) (i) Kishazi ni kipashio au kifungu chochote katika sentensi chenye kitenzi. (alama 2)
(ii) Alipofika – tegemezi
Alipumzika – huru (alama 2)

(e) (i) Kara'tasi
(ii) 'Mama (alama 2)

(f) Ukilipa ingia ndani. (alama 2)

(g) <u>Udogo</u>
Kibuzi kiliuawa na kijizi hicho (alama 2)
<u>Ukubwa</u>
Buzi liliuawa na jizi hilo. (alama 2)
Zozote 2 x 1 = alama 2

(h) /j/ /ch/ /ny/ /sh/ /y/

(i) (a) Nge – A – WA
(b) Gofu – LI – YA (alama 2)

(j) Mwanafunzi achelewaye huadhibiwa
* Lazima mwanafunzi atumie "O" rejeshi tamati (alama 2)

(k) "Tafadhali Mutiso njoo hapa nikutume." Juma akaomba. (alama 3)

(l) (i) Hadaa – danganya
(ii) Andaa – tayarisha (alama 2)

(m) (i) Nomino – Ndoa yao ilikuwa na <u>ila</u> ndiposa ilivunjika.
(ii) Kiunganishi – Niliamka mapema <u>ila</u> sikumpata. (alama 2)

(n) (i) Mamba – ngwena
(ii) Mviringo – duara (alama 2)

(o) (i) Taarifa – arifu
(ii) Msamaha – samehe, samehea
(iii) Toba – tubu (3 x 1 = alama 3)

(p) (i) Mahali huku kuna wadudu wengi.
(ii) Mahala hapa pana wadudu wengi.
(iii) Mahali humu mna wadudu wengi.
(Yoyote 1 x 1 = alama 1)

Utuzaji
- Adhibu makosa ya hijai yanapotokea mara ya kwanza hadi makosa 6. (alama 3)
- Adhibu makosa ya sarufi yanapotokea kwa mara ya kwanza bora usiadhibu zaidi ya nusu ya alama zilizotuzwa.

4. **<u>ISIMU JAMII</u>**
- Dini.
- Biashara.
- Mafunzo na utahini shuleni.
- Vyombo vya habari.
- Ndoa baina ya watu wa jamii tofauti.
- Siasa.

- Uandishi wa vitabu na majarida.
- Chombo cha utawala
- Mijadala na hotuba.
- Bunge.
- Kufanywa lugha ya taifa / rasmi (katiba mpya)

Utuzaji

Hijai

Adhibu makosa ya hijai (h) yanapotokea mara ya kwanza hadi makosa sita (alama 3)

Sarufi

Adhibu makosa ya sarufi (s) yanapotokea kwa mara ya kwanza bora usiadhibu zaidi ya nusu ya alama zilizotuzwa.

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mwanafunzi _____

Tarehe _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA: 2 ½

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3
MUDA : 2 ½

MAAGIZO
(a) Jibu maswali MANNE pekee.
(b) Swali la kwanza ni la lazima.
(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na ushairi.
(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

Kijitabu hiki kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

SEHEMU A: (SWALI LA KWANZA LA LAZIMA)

1. (a) Taja sifa zozote nne za maigizo. (alama 2)
   (b) Taja aina zozote nne za maigizo. (lama 2)
   (c) Ni nini tofauti ya maagizo na hadithi. (alama 10)
   (d) Eleza dhima ya maigizo kama utanzu wa fasihi simulizi. (alama 6)

SEHEMU YA B: (TAMTHILIA) KIFO KISIMANI NA KITHAKA WA MBERIA.

2. "Hatuna chuki na Mtemi wa Butangi wala na mtu mwingine tena."
   (a) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza tofauti zilizoelezwa na anayezungumziwa kuhusu uongozi wa awali na wa sasa. (alama 6)

3. Tofauti na mtazamo wa watu wengi, mwanamke katika Butangi amesawiriwa kwa lengo la kuinua hadhi yake. Kwa kurejelea tamthlia ya Kifo Kisimani, thibitisha ukweli wa kauli hii.

SEHEMU YA C – RIWAYA (UTENGANO) SAID A MOHAMED.

4. " Mama usifanye mchezo hivyo. Ikiwa ni kuvunja miiko ya nyumba hii tusiogope, naivunjwe leo hiyo miiko".
   (a) Eleza mktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Fafanua miiko iliyorejelewa katika dondoo hili. (alama 8)
   (c) Je, miiko hii ilivunjwa na matokeo yalikuwa yapi. (alama 8)

SEHEMU YA D (Hadithi fupi)

Mayai Waziri na maradhi na hadithi nyingine k.w. Wamitila.

5. "Sekta ya Elimu ina matatizo mengi sana." Huku ukizingatia hadithi zozote tano katika diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi, eleza kauli hii.

6. (a) Ukumi katika hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi umetajwa kwa maana mbalimbali. Zitaje na ufafanue. (alama 8)

   (b) Hadithi hii ya Mayai Waziri wa Maradhi inamulika matatizo ya nchi za Afrika baada ya uhuru. Jadili. (alama 12)

SEHEMU YA E: USHAIRI

7. Soma mashairi haya kisha ujibu maswali.

1. Upendacho hupendeza, japo kibaya machoni,
   Hakiwi kukuchukiza, pendo liwapo moyoni.
   Pofu huita kengeza, watu wakaona shani,
   Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

2. Wajao kukuliza, nduguzo na majirani,
   Mtu huyo ameoza, macho yake hayaoni,
   Budi utawajibiza, yangu yawahusiani,
   Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

3. Sababu zao bugudha, hutaki nao utani,
Kujua hapana ndha, ya mtu ila rohoni,
Ni hali ghani orodha, isiyo na wakikini,
Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

4. Kingawaje maridhawa, kitukufu kwa thamani,
Ni hali yenye usawa, maisha hasitawani,
Moyo unapochopotowa, tajiri na maskini,
Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

B

1. Lau kwamba waelewa, lililo langu moyoni
Katu hungalitobowa, kueleza hadharani
Apendaye hana dawa, mwenye hupenda haoni

2. Haoni na hasikii, hafui wala hashoni
Hendi wala hakimbii, haogi na hatamani
Kezuia kii kii, wangasema majirani.

3. Majirani wangenena, humtia midomoni.
Na hata habari hana, msemayo asilani
Yuko tuli amebana, awatazama machoni.

4. Machoni awatazama, kuwajibu katwaani
Ni bure mngasema, mwajiudhi ikhiwani
Basi hapa kaditama, ndugu zangu kwaherini.

Maswali

(a) Pendekeza anwani kwa shairi la A. (alama 2)

(b) Jadili mashairi haya kiarudhi. (alama 6)

(c) Mafungu haya yana maana gani kama yalivyotumika katika mashairi haya. (alama 2)
(i) Budi utawajibiza, yangu yawahusiani?
(ii) Sababu zao bugudha, hutaki nao utani.

(d) Andika methali zinazorejelewa na ueleze maana yake. (alama 3)

(e) Andika ubeti wa tatu wa shairi la B katika lugha ya nathari. (alama 2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama yalivyotumika katika mashairi yote mawili. (alama 3)
(i) Shani
(ii) Maridhawa
(iii) Asilani

(g) Kwa kurejelea ubeti wa pili wa shairi A, onyesha jinsi mwandishi amezingatia uhuru wa kishairi. (alama 2)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011

KANGUNDO DISTRICT FORM FOUR MULTILATERAL EXAM
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1. (i) Yanaambatana na mambo ya dhati katika maisha ya mwanadamu kama vile arusi, matanga n.k.
(ii) Yana mpito wa wakati kwa mfano sherehe za jando zinamtoa mvulana utoto na kumwingiza katika rika la utu uzima.
(iii) Mara nyingine hutumia maleba na mapiku.
(iv) Matendo hujitokeza bayana; huwa na mazingira na nafasi ya kuonyesha wazi kama vile tabia, mielekeo, malezi na vipawa asilia vya watoto wa jamii.
(v) Yana ujenzi wa uzoefu wa maisha kwa marika mbalimbali.
(vi) Yanafundisha watu kuishi pamoja.
(vii) Utendaji husheheni nyimbo, masimulizi ngoma, lugha teule k.m mafumbo na hata istiara.
(viii) Wachezaji na hadhira kwa kawaida huwa ni wale wanaoshiriki katika maigizo.
Alama 4 x ½ = 2

(b) (i) Mazungumzo
(ii) Majigambo
(iii) Michezo
(iv) Vichekesho
(v) Miviga
(vi) Jando
(vii) Unyago
(viii) Ngonjera alama 4 x ½ = 2

MAIGIZO	HADITHI
1. Huambatana na mambo ya dhati ya maisha ya mwanadamu k.v arusi, matanga, jando, unyago	1. Aghalabu husheheni mambo ya kufikiria au kubuni kuanzia wahusika hadi visa vyenyewe.
2. Yana mapito ya wakati k.m Sherehe za jando zinamtoa mvulana utotoni na kumwingiza hadi rika la utu uzima.	2. Hadithi mara nyingi hazina mipaka ya rika au kufunza mtu kutoka rika moja hadi lingine.
3. Maigizo – Mada zake huhusu matokeo ya kila siku maishani k.v ndoa, jando n.k	3. Hadithi huhusu mambo ya zamani au ya kubuni ambayo hayako katika uhalisia.
4. Hakuna matayarisho ya awali hutokea kulingana na mazingira au haja, maneno na matendo huzuiliwa papo kwa papo	4. Mara nyingi huwa jioni baada ya kazi na mtambaji hujitayarisha kwa wakati huu.
5. Mianzo ya maigizo hutegemea kinachoigizwa k.m arusi, nyimbo, tanzia, kilio n.k	5. Hadithi huwa na mianzo maalum k.v paukwa pakawa!
6. Matendo ya kiasilia kihalisi na hapana hoja ya ufaraguzi.	6. Hadithi hutegemea ufaraguzi kwa upande wa mtambaji ili kunata hadhira na kupasha ujumbe kwa njia mwafaka zaidi.

Alama 5 x 2 = 10

(c) (i) Huburudisha wanajamii kama vile michezo, vichekesho.
(ii) Kupitia kwa Jando, unyago na mazungumzo mafunzo ya kiutu uzima yalitolewa kwa vijana ama vile maadili.mila na desturi.
(iii) Maigizo yalikuwa vipawa vya kazi mbalimbali miongoni mwa wanajamii kwa mfano usasi, ukulima, usonora, utuaji, uvuvi n.k
(iv) Maigizo yalionyesha mpito wa wakati k.v unyago, jando, mazishi, arusi n.k
(v) Maigizo yaliweza kufunza na kutenga majukumu kati ya wanajamii mbalimbali.
(vi) Maigizo yalidhimisha utamaduni wa jamii husika kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Alama 6

2. Mkutadha wa dondoo hili
(i)Ni mtiririko wa mawazo ya Gege akizungumza na Mwelusi. (alama2)
(ii) Akiwa nyumbani / uani mwa Tanya . (alama 1)
(iii) Wakati ambapo Tanya anamhimiza aende kumtembelea nduguye gerezani ndipo akakumbuka mazungumzo baina yake na Mwelusi. (alama 1)

UONGOZI WA AWALI WA MTEMI MLIMA	UONGOZI WA SASA WA MTEMI BOKONO
(i) Mazingira bora	(i) Mazingira yameharibika
(ii) Chemichemi zilikuwa na maji	(ii) Chemichemi zilikuwa zimekauka
(iii) Udongo wenye rotuba	(iii) Rotuba imebebwa na maji baada ya ukataji wa miti.
(iv) Shibe – mapato na mazao ya kutosha.	(iv) Njaa
(v) Vilima vya Butangi vilikuwa na afya njema. Vilifunikwa na miti mirefu, mitambazi na nyasi.	(v) Mmomonyoko wa ardhi umeadhiri vilima
(vi) Usalama ulidumishwa kwa wananchi	(vi) Wananchi hawana usalama
(vii) Watawala hawakuwa wanalima na kufunga ng'ombe popote	(vii) Watawala wanalima na kufunga ng'ombe popote
(viii) Hakukuwa na ubaguzi wa wanavijiji	(viii) Kuna ubaguzi wa wanavijiji
(ix) Kulikuwa na haki, usawa na maendeleo	(ix) Hakuna haki, usawa na maendeleo
(x) Raslimali za nchi zilitumiwa na wote.	(x) Raslimali za nchi zinatumiwa na wachache

8 x 2 = alama 16

3. Katika tamthilia ya Kifo Kisimani, mwanamke amepewa nafasi nzuri, hajabaguliwa.
(i) Amechorwa kama kiumbe mwenye maadili mema na mlezi wa kusifika kwa mfano, Tanya amewalea wanawe vizuri licha ya kuwa mjane.
(ii) Wanawake ni wenyenyekevu na wapole. Tanya anamnyenyekea askari ili wamruhusu amwone mwanawe Mwelusi.
(iii) Ni wavumilivu na wenye roho safi licha ya kutukanwa na mumewe, Nyalwe anaendelea kuuliza kinachomuumiza.
(iv) Hawana hulka ya woga. Wamejitokeza wazi kutetea haki zao mfano, Andua anakabiliana vikali na askari wanaomkataza ampe Mwelusi chakula. Pia kwa ujasiri anaenda kisimani na kuvunja kanuni iliyowekwa kukanyaga mchanga wa Bonde la Ilangi.
(v) Ni viumbe wenye bidii mfano Kaloo anafika mapema kuandaa jukwaa Mtemi atakalo hutubia.
(vi) Ni wasaidizi – Azena anakuja kumjulia hali Tanya na kumpa mawaidha asikate tamaa.
(vii) Ni wenye busara – Busara yao inawafanya wapewe majukumu katika uongozi mfano Mama Agoro anayewakilisha watu kutetea ardhi yao.
(viii) Wamepevuka na kujua haki zao ambazo wanazitetea bila kufa moyo.
(ix) Wenye huruma – Tanya anamsikitikia mwanawe Mwelusi aliyetiwa gerezani. Nyalwe naye Anamhurumia mumewe kutokana na hali iliyomkumba.
(x) Ni wazalendo halisi – Wako katika mstari wa mbele katika ukombozi na mapinduzi huko Butangi kupigania haki za wanabutangi.
(xi) Ni vipao mbele katika ukombozi na mapinduzi huko Butangi mfano Atega, Andua, Azena na wengine wengi wanaoongoza hadi ikulu ya Mtemi Bokono.

(alama 10 x 2 = 20)

4. (a)(i) Anayezungumza ni Maimuna
(ii) Anamwambia mama yake Bi. Tamima
(iii) Nyumbani kwa Bwana Maksuudi
(iv) Bi. Tamima alikuwa mjamzito, akapiga kite kuhisi kujifungua. Maksuudi hakuwa nyumbani na Tamima alihitaji msaada wa kupelekwa hospitalini bali kulikuwa na masharti aliyowekewa na Maksuudi. Hapa Maimuna alijawa na huzuni na kumsihi mamake wavunje miiko waliowekewa na Maksuudi.

(4 x 1 = alama 4

(b) Miiko
(i) Kutawishwa – Hawakuwa na ruhusa ya kutoka nje bila idhini yake(Tamima na Bintiye)
(ii) Kutokuwa na uhuru wa kujiamulia lolote hata kama maisha yao yamo hatarini (Tamima na Butiye)
(iii) Idhini na amri zote ni kutoka kwa Maksuudi.
(iv) Hakuna ruhusa ya kutoka na kutangamana na wengine.
(v) Hakuna ruhusa ya wageni / mtu yeyote kuingia kwa boma la Maksuudi. (Mkunga)
(vi) Taa kuzimwa mapema.

4 x 2 = alama 8

(c) Ndiyo miiko ilivunjwa na Maimuna na Biti-kocho 4 x 2 = alama 8

Mwanafunzi aelezee hoja

Matokeo ya miiko kuvunjwa
(i) Kutoroka kwa Maimuna
(ii) Kichapo cha Tamima
(iii) Kutalikiwa kwa Tamima
(iv) Kufutwa kazi kwa Kocho
(v) Kifo cha mtoto mchanga

4 x 2 = alama 8
Mwanafunzi aelezee hoja

6. (i) NDIMI ZA MAUTI
(i) Uongozi mbaya – Wanafunzi kukaziwa
(ii) Vurugu shuleni
(iii) Vifo vya wanafunzi
(iv) Waalimu kulaumiwa kwa matatizo yoyote
(v) Kukosa vifaa vya kupambana / kukabiliana na mikasa

(ii) FUMBO LA MWANA
(i) Dawa za kulevya
(ii) Ajira ya watoto
(iii) Ukosefu wa karo / ulipaji wa karo / umaskini
(iv) Kutowajibika kwa wazazi
(v) Jamii kutowajibika / malezi mabaya

4 x 1 = alama 4

(iii) NGOME YA NAFSI
(i) Ndoa za mapema – wasichana kuachishwa shule
(ii) Ndoa za lazima
(iii) Madawa ya kulevya – Idi
(iv) Imani ya jamii kubagua wasichana wasisome. 4 x 1 = alama 4

(iv) UTEUZI WA MOYONI
(i) Ndoa za mapema
(ii) Ndoa za lazima
(iii) Wasichana kubaguliwa kielimu
(iv) Watu kusoma na kukosa kazi – Zena kufungua kibanda
(v) Umaskini – Milango ya shule kwa taabu mno

4 x 1 = alama 4

(v) KACHUKUA HATUA
(i) Umaskini
(ii) Mimba za mapema
(iii) Ajira ya watoto
(iv) Kutowajibika / dharau za waalimu
(v) Kutowajibika kwa wazazi

4 x 1 = alama 4

(i) Watoto kumi waliozaliwa siku ya uhuru.
(ii) Watoto kumi waliokondeana wakimjia waziri Mayai usingizini.
(iii) Maendeleo ya miaka kumi.
(iv) Ukombozi kurudi nyumbani saa kumi.
(v) Sherehe za miaka kumi.
(vi) Morris kupiga ngoma kumi.

4 x 2 = alama 8

(b) Matatizo ya nchi za Afrika.
(i) Uwajibikaji wa viongozi – viongozi wasiwajibika .
(ii) Ufisadi.
(iii) Viongozi kuwadhulumu wananchi – Kukojolea mito .
(iv) Ubinafsi
(v) Ubadhirifu wa viongozi
(vi) Njaa
(vii) Umaskini
(viii) Ukoloni mamboleo
(ix) Katika vielelezo Mwanafunzi aeleze hoja

6 x 2 = alama 12

SEHEMU YA E: USHAIRI

7. (a) Kipendacho moyo / upofu wa mapenzi. (alama 2)

(b) Shairi la A
(i) Tarbia – lina mishororo minne
(ii) Lina mizani 16 kila mshororo
(iii) Lina beti nne
(iv) Vina vya ndani vinatiririka na vya nje vinatofautiana
(v) Mshororo wa mwisho umerudiwarudiwa

Shairi la B
(i) Tathlitha (mishororo tatu)
(ii) Mizani 10 kila mshororo
(iii) Lina beti nne
(iv) Vina vya nje vinatiririka vya ndani vinatofautiana
(v) Mshororo wa mwisho unatofautiana

Alama 3 x 2 = 6

(c) (i) Anawajibu kwamba mambo yake yanawahusu nini (alama 1)
(ii) Anaonelea kuwa sababu wanazotoa ni za kuwaudhi tu. (alama 1)

(d) (i) Kipendacho moyo dawa : kile akipendacho mtu huwa ni kama dawa yake.
(ii) Apendaye hana dawa : Mtu anapopenda kitu hakuna lolote linaloweza kuzuia mapenzi yao.
(iii) Mwenye kupenda haoni : Mtu ambaye anapenda kitu ni kama kipofu, mawazo yake yamepotoshwa.

(alama 3)

(e) Majirani wanapozungumza humsengenya ilhali hajui wasemayo kabisa, amenyamaza kimya akiwaangalia.

(alama 2)

(f) (i) Ajabu
(ii) Ridhisha / pendekeza
(iii) Kamwe / kabisa

(g) Inkisari
Mifano
(i) Nduguzo – Ndugu zako.
(ii) Yawahusiani – Yawahusu nini

(alama 2)